TANGAZO LA SERIKALI Namba 322 la tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6 (1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA YA VIBALI VYA BURUDANI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI, 2010

Jina na mwanzo wa kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada ya Vibali vya Burdani) za Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Ada" maana yake ni kiwango cha fedha kitakachopangwa na Halmashauri na kutozwa katika vibali vya Burdani isipokuwa ile ya kiserikali na madhehebu ya Kidini.

"Afisa Mtendaji" maana yake ni Afisa Mtendaji Kata au Mtaa katika Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji na usimamizi wa Sheria Ndogo hizi.

"Afisa Utamaduni" maana yake ni Afisa Utamadani wa Halmashauri.

"Burudani" maana yake ni tukio ambalo litakuwa linafanyika kwa kukusanya watu mbalimbali katika ukumbi, uwanja au eneo lolote litakalo ruhusiwa na Halmashauri

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya

Mkurugenzi.

"Sherehe" maana yake ni tukio la mkusanyiko wa watu zaidi ya watu ishirini na kufanyika katika ukumbi, mtaa, uwanja au enco lolote litakaoruhusiwa na Halmashauri.

"Ukumbi wa Video" maana yake ni jengo lolote lililoidhinishwa na Halmashauri kwa kuonyesha Video.

"Video na Sinema" maana yake ni picha zozote zinazoonyeshwa katika kumbi za Video na Sinema na zenye maadili.

Kibali

4 (1) Mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali au Kidini itakayotaka kuendesha Burdani, Sherehe, Video au Sinema katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuomba na kupata kibali cha kuendeshea shughuli hiyo toka Halmashauri.

(2) Kibali hicho kitalipiwa ada kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Kibali hicho kitaonyesha;-

(a) sehemu itakayofanyika shughuli hiyo.

(b) Muda wa kuanzia na kuishia shughuli hiyo

(4) Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatanisho vyote vinavyohusika

5 Itakuwa ni marufuku kwa mmiliki wa ukumbi wa Video na Sinema au sehemu yoyote iliyoruhusiwa kuonyesha picha za Video kuonyesha picha ambazo zinakiuka maadili.

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

6 Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa;-

(a) kuingia katika Ukumbi wowote wa Burdani, Sinema au Sherehe yeyote inayofanyika katika Mtaa au hadharani kukagua kibali kinachoruhusu uendeshaji wa shughuli hiyo.

(b) kufunga shughuli yoyote endapo shughuli hiyo inakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha kufunga barabara

7 Itakuwa ni wajibu wa mtu yeyote au kikundi cha watu kitakachofanya sherehe katika mitaa kuomba kibali cha kufunga barabara ya mtaa na kutalipa ada ya kufunga barabara au mtaa

kama ilivyoonyesha kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu 8 Mtu au Taasisi au kikundi chochote atakayekwenda au kukiuka Kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa Mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miaka miwili (2) jela au adhabu zote kwa pamoja faini na kifungo.

Kufifilisha kosa 9 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu au Taasisi yeyote itakayokwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji atakiri kutenda kosa kwa maandishi na kukubali kulipa ada anayodaiwa. Faini itozwayo haitazidi ile iliyoko katika kifungu (8) cha Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI

Na.	Aina ya shughuli	Kiwango cha Ada kwa onyesho
1.	Muziki wa Dansi	50,000/=
2.	Muziki wa Disco	50,000/=
3.	Promotion	50,000/=
4.	Shindano la kutafuta msanii	50,000/=
5.	Shindano la kutafuta Warembo	50,000/=
6.	Maonyesha ya Mavazi	20,000/=
7.	Shindano la Mpira	20,000 Mechi za nje 5,000 Mechi za ndani
8.	Muziki wa Taarabu	20,000/=
9.	Muziki wa Asili	10,000/=
10.	Ngoma za Asili	5,000/=
11.	Sherehe ya Harusi	20,000/=
12.	Mchiriku	5,000/=
13.	Maonyesho ya Sinema na Video	5,000/= kila siku
14.	Wapiga picha za Video	20,000/=
15.	Kufunga barabara ya Mtaani	20,000/= kwa masaa manne

Nembo ya Halmashauri imebandikiwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia Azimio la Kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 31 Julai, 2009

Nembo hiyo imebandikwa mbele ya:-

LEWIS. K. KALINJUNA
Mkurugenzi
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

SHABANI MAMBO
Naibu Mstahiki Meya
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

NAKUBALI

MHE. MIZENGO. P. PINDA
WAZIRI MKUU

DODOMA. 29/7/2011